

Maswali

1. Daudi alijificha wapi alipotoroka kutoka kwa Sauli?
2. Watu wangapi walikuja kuwa na Daudi?
3. Nabali alikuwa na kondoo na mbuzi wangapi?
4. Watu wa Daudi walienda kuuliza Nabali nini?
5. Daudi alikasirika sana wakati Nabali alisema hawangepata chakula. Daudi alipanga kufanya nini?
6. Nani alienda kupea Daudi chakula na kumsihi asiue Nabali?
7. Daudi aliambia Abigaili nini alipowaletea chakula na kuwasihi wasiue Nabali?
8. Nini ilifanyika baada ya Nabali kufa?

Majibu

1. Pangoni.
2. Wanaume 400 lakini wakaongezeka mpaka 600.
3. Kondoo 3000 na mbuzi 1000.
4. Waliuliza chakula.
5. Alipanga kuenda amue Nabali.
6. Abigaili.
7. Kwamba alikuwa mwanamke mwerevu.
8. Daudi alimuoa Abigaili.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



16 Daudi na Abigaili

Marejeo

1 Samweli 25

Kiini cha somo

Furahia hukumu nzuri.


Maneno maalum

1. Daudi alificha + Wanaume 400 + familia ya Daudi + mfalme wa Moabu + wanaume 600.
2. Nabali + tajiri + mchoyo + Abigaili + mrembo + hekima (Busara).
3. Daudi + kinga + kata kondoo manyoya + siku ya karamu + omba chakula.
4. Nabali akakataa + Daudi anakasirika + ua Nabali.
5. Watumishi + Abigaili + chakula + Daudi.
6. Daudi ashukuru + Nabali akafa + Daudi akamuoa Abigaili.

16.1 Abigail alikuwa mwanamke wa busara. Alizuia Daudi kufanya makosa. Daudi alipotoroka kutoka kwa Sauli, alijificha katika pango. Ndugu zake pamoja na familia yake walijiunga naye na akawa kiongozi wao. Daudi alienda kwa mfalme wa Moabu na akamuuliza, “Tafadhali kubali baba na mama wangu waishi na wewe mpaka nione kitakachofanyika kwangu.” Ikiwa hivyo. Daudi na watu wake wakaenda kujificha.

16.2 Ilikuwa baada ya hayo ndio Daudi alikutana na Abigail. Mmewe aliitwa Nabali, naye alikuwa tajiri na shamba kubwa. Alikuwa na kondoo 3000 na mbuzi 1000. Alikuwa na kiburi tena mchoyo. Lakini Abigail alikuwa mrembo na mwenye busara.


Alijua alichokuwa akifanya na hata aliokoa familia yake. Hebu tuone vile ilikuwa.



16.3 Daudi na watu wake walikuwa wamejificha kwa shamba la Nabali na walikuwa wazuri kwake. Walimlindia kondoo wake kwa hivyo Daudi alituma watu wake kwa Nabali ili awasaidie. Watu wa Daudi walimuendea wakati Nabali na watu wake walikuwa wanakata manyoya ya kondoo. Ilikuwa wakati wa karamu kwa hivyo kulikuwa na vitu vingi vya kukula. Watu wa Daudi walisema hivi, “Tumekuwa wazuri kwako. Hatukuiba kondoo wako na hata tulisaidia kuwalinda. Tafadhali tusaidie chakula.”



16.4 Nabali alisema, “Siwezi kuwapa watu kama nyinyi chakula.” Alizungumza maneno mbaya sana ya kiburi juu ya Daudi. Watu wake walipomwambia Daudi, Daudi alikasirika sana. Akawambia, “Chukuwa mapanga!” Walianza safari ili waende waue Nabali na watu wake.



16.5 Mmoja wa watu wa Nabali aliyesikia alichosema kwa watu wa Daudi, alienda akamwambia Abigail kilichokuweco. Punde tu, Abigail alitengeneza chakula

akapakia juu ya punda wake na akaenda kumuona Daudi. Alipokutana nae aliteremka kutoka kwa punda na kuinama chini kwa heshima. Akasema, “Tafadhali bwana wangu usimwangelie mme wangu Nabali, nimjinga na kila wakati anafanya ujinga. Nimekuletea zawadi, tafadhali ichukue na, utusamehe yote yaliyotendeka.”

16.6 Daudi alijibu, “Wewe ni mwanamke mwerevu. Umenizuia kulipisha kisasi kwa Nabali kwa uchoyo wake. Sitamua. Rudi nyumbani kwa amani. Baadaye Nabali alipokuwa amekufa Abigail akawa mmoja wa wake wa Daudi.

